



# NISHATI

HABARI ZA  
NISHATI

## News **Bulletin**

[www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz) Wizara ya Nishati wizara\_ya\_nishati\_tanzania @Nishati2017 Wizara ya Nishati

Toleo Namba 43

Oktoba 1 - 31, 2022

# Serikali inaendelea na ujenzi wa Bomba la Mafuta-Majaliwa



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa



**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA  
MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au  
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma

# BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**  
**Mhandisi Felchesmi Mramba**  
Katibu Mkuu

**Makamu Mwenyekiti**  
**Kheri Mahimbali**

**Mhariri**  
**Dorina G. Makaya**

**Waandishi**  
Teresia Mhagama  
Zuena Msuya  
Hafsa Omar  
Timotheo Mathayo

**Msanifu Kurasa**  
Lucas Gordon


**Wasiliana nasi kwa simu**  
**namba +255-26-2322018**  
**Nukushi: +255-26-2320148**  
au


**Fika Ofisi ya Mawasiliano**  
Mitumba Dodoma,  
S.L.P 2494, Dodoma

 [www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz)

 [Wizara ya Nishati](#)

 [@Nishati2017](#)

 [wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](#)

 [Wizara ya Nishati](#)

## UNITED REPUBLIC OF TANZANIA MINISTRY OF ENERGY



### GOVERNMENT STATEMENT AGAINST EUROPEAN UNION PARLIAMENT RESOLUTION ON EACOP PROJECT.

On 15<sup>th</sup> September 2022, the European Union Parliament made a resolution number P9\_TA (2022) 0321 on the matters relating to the **Human Rights** and **Environmental Concerns** posed by the implementation of the EACOP Project in Uganda and Tanzania.

Tanzania being one of the Shareholders to the EACOP Project is seriously concerned by grave factual misrepresentations in the resolution issued by EU Parliament. In view of that, the Government wishes to issues the following clarifications:

- The EACOP Project is being implemented with strict observance of International Safety, Environmental and Social aspects, including Human Rights. To demonstrate this adherence in the Project, a dedicated Human Rights Impact Assessment (HRIA) was undertaken as part of the project implementation process. The HRIA assessed and put in place measures for addressing the potential adverse effects of the Project on the human rights enjoyment.
- Equally, the Project Environmental and Social Impact Assessment (ESIA) process was adequately undertaken and approved by the relevant Environmental Management bodies including the National Environmental Management Council (NEMC). Notably, ESIA identified comprehensive and adequate measures to safeguard environmental sustainability during and post project construction.
- It is paramount to underscore the fact that the Pipeline route is designed to minimize Environmental and Social impacts as well as physical displacement and render low economic impacts to nearby communities. To exhibit this Project fact, there are 9,513 Project Affected Persons (PAPs – *broadly corresponding to households and including commercial and government institutions*). Out of these, it was only 331 PAPs displaced (which represents 3.5% of total Project affected Persons) against 100,000 claimed by the EU resolution as being displaced.
- Displaced PAPs are offered a choice between replacement housing or cash compensation. Over 85% of the physically displaced PAPs have opted for replacement housing. Construction of these houses has started and out of 309 houses: 37 have been completed and handed over, 55 are on completion stage and 217 are on initial construction stage.
- Furthermore, the project land acquisition process (Compensation, Resettlement, Livelihood Restoration and Transition Support.) was carried out in compliant with both the Laws of Tanzania and the Performance Standards of the International Finance Corporation (IFC) as verified by Lenders Environmental and Social Consultant (LESC).
- In compliance, all basic principles of compensation including treating each PAP with respect and compensating each PAP at **full replacement value** is the norm of the Resettlement exercise. The Government of Tanzania and the Project company agreed in principle that, **no land will be accessed by the project until compensation and resettlement has been fully undertaken and notice to vacate has been issued**. This has been the norm of this Project and intensely monitored by the Government.

The Government of Tanzania wishes to assure all Stakeholders including the European Union Parliament and the entire International Community that, EACOP Project is being implemented in line with Best Industry Practices in terms of transparency, Environmental, Social, Gender Inclusiveness and Human Rights considerations with the aim of ushering shared prosperity and sustainable development to its citizens.

Issued by the Ministry of Energy.  
19<sup>th</sup> September 2022



# Serikali inaendelea na ujenzi wa Bomba la Mafuta-Majaliwa

**W**aziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa amesema Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan inasimamia kikamilifu Sekta ya Nishati ikiwemo kuendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani Tanga nchini Tanzania ili kukuza uchumi.

Waziri Mkuu aliyasema hayo (Ijumaa, Septemba 23, 2022) wakati akiahirisha Mkutano wa Nane wa Bunge la 12, bungeni jijini Dodoma. Alisema baadhi ya wadau wa maendeleo wamekuwa na mashaka katika utekelezaji wa mradi huo wakihofia kuwa unaweza kutekelezwa pasipo kuzingatia athari za kimazingira na haki za binadamu.

Hata hivyo, Mheshimiwa Majaliwa alisisitiza kuwa, mradi huo umefanyiwa tathmini ya kina ya kimazingira na kuhakikisha kuwa utekelezaji wake hauna athari za kimazingira

na kwa jamii. "Mradi huu kwa upande wa Tanzania unagusa watu 9,513 ikiwemo taasisi mbalimbali. Miongoni mwao ni watu 331 pekee ndio watakaohamishwa sawa na asilimia 3.5." Alisisitiza

Waziri Mkuu aliongeza kuwa wanaoguswa na mradi huo walishirikishwa kuchagua kujengewa makazi mapya au kupewa fedha taslimu. Hata hivyo asilimia 85 walichagua kujengewa makazi na ujenzi wa makazi hayo unaendelea ambapo nyumba 37 kati ya 309 zimekamilika na kukabidhiwa kwa wahusika. Aidha, nyumba 55 zipo kwenye hatua ya umaliziaji na nyumba 217 zipo kwenye hatua za awali za ujenzi.

Alisema Serikali ya Tanzania inaungana na Serikali ya Uganda kuwahakikishia wadau wote likiwemo Bunge la Umoja wa Ulaya na Jumuiya ya Kimataifa kuwa mradi huo unatekelezwa kwa kuzingatia sheria zote za Tanzania na za Kimataifa, uwazi, tahadhari za kimazingira, ulinzi wa mifumo ya kiikolojia na rasilimali za maji,



Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa

masuala ya kijamii, kijinsia na haki za binadamu kwa ujumla.

Aliongeza kuwa, "Mradi huu ni muhimu kwa manufaa ya nchi zetu mbili katika kukuza biashara, viwanda vya uzalishaji, kuongeza ajira pamoja na kuvutia wawekezaji ambao wanatarajia kukuza teknolojia na ujuzi kwa wananchi. Mheshimiwa Rais ana matamano mabwa ya kuifanya sekta ya nishati kuwa chanzo cha ukuaji wa

uchumi na kuboresha sekta nyingine ikiwemo viwanda ambavyo ukuaji wake unategemea zaidi uwepo wa nishati ikiwemo mafuta na gesi."

"Hivyo niwatoe hofu wadau wote kuhusiana na utekelezaji wa mradi huu na Serikali itaendelea kutumia njia za kidiplomasia kuhakikisha wadau wanapata taarifa sahihi kuhusu utekelezaji wa mradi na uzingatiaji wa viwango vya Kimataifa." Alisema



# WAZIRI MAKAMBA AMWAKILISHA RAIS SAMIA UHOLANZI

**W**aziri wa Nishati, Mhe. January Makamba amemwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, kwenye Mkutano wa Viongozi wa Dunia unaojadili Programu ya Afrika ya kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (Africa Adaptation Summit) uliofanyika Rotterdam, Uholanz tarehe 5/9/2022.

Mkutano huo ulilenga kushawishi Washirika wa Maendeleo, Taasisi za Kifedha na Sekta binafsi na marafiki wa Afrika kuchangia fedha kwenye Programu hiyo ya Afrika ambayo inahitaji Dola za Marekani Bilioni 25 ifikapo 2025. Benki ya Maendeleo ya Afrika imechangia Dola za Marekani bilioni 12.5.

Mkutano huo umefanyika kama sehemu ya maandalizi ya mkutano wa 27 nchi wananchama wa mkataba wa mabadiliko ya Tabianchi ambao unatarajiwa kufanyika mwezi Novemba mwaka



*Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba akiwa katika Mkutano wa Viongozi wa Dunia unaojadili Programu ya Afrika ya kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (Africa Adaptation Summit) uliofanyika Rotterdam, Uholanzi tarehe 5/9/2022. Waziri Makamba alimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwenye Mkutano huo.*



*Sehemu ya Washiriki wa Mkutano wa Viongozi wa Dunia unaojadili Programu ya Afrika ya kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (Africa Adaptation Summit) unaofanyika Rotterdam, Uholanzi tarehe 5/9/2022. Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba amemwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, kwenye mkutano huo.*



# WAZIRI MAKAMBA AMWAKILISHA RAIS SAMIA UHOLANZI

huu huko Sharm El Sheik Misri ambako suala la kuhimili mabadiko ya Tabianchi kwa Afrika ni moja ya ajenda muhimu za mkutano huo.

Katika Mkutano huo, Waziri wa Nishati alikutana na Viongozi wa Dunia, Wakuu wa Taasisi na Mashirika mbalimbali na kujadiliana nao fursa mbalimbali ikiwa pamoja na namna bora ya Tanzania kunufaika na mpango huo wa AFRICA ADAPTATION ACCELERATION PROGRAM (AAP) ambao utaharakisha



Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba akizungumza katika Mkutano wa Viongozi wa Dunia unaojadili Programu ya Afrika ya kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (Africa Adaptation Summit) uliofanyika Rotterdam, Uholanzi tarehe 5/9/2022. Waziri Makamba alimwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwenye Mkutano huo.



Waziri wa Nishati Mhe. January Makamba akijadili jambo na Mkurugenzi Mkuu Shirika la Fedha Duniani, Kristalina Georgieva baada ya Mkutano wa Viongozi wa Dunia wa mabadiliko ya tabianchi kwa Afrika.

mipango ya nchi katika kukabiliana na majanga yakiwemo UVIK019, ukame, njaa, ajira kwa vijana na mafuriko.

Mkutano huo uliongozwa na Rais wa Jamhuri ya Senegal na Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika, Mhe. Macky Sally, na Katibu Mkuu Mstaafu wa Umoja wa Mataifa pia Mwenyekiti wa Kituo cha kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (GCA) Mhe. Ban Ki-Moon.



# SERIKALI YAAHIDI KUJENGA VITUO 15 VYA KUPOZA UMEME

**Na Godfrey Mwemezi, Dodoma.**

**S**erikali inaendelea na mchakato wa kujenga vituo vya kupoza umeme katika maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika.

Kauli hiyo imetolewa na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato alipokuwa akizungumza kwenye

semina ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) iliyofanyika jijini Dodoma.

Alisema, vituo 15 vya kupoza umeme vinatarajiwa kujengwa kwa mwaka 2022/2023 na vipo kwenye mpango wa gridi imara, ambapo taratibu za kuwapata wakandarasi wajenzi wa vituo hivyo zinaendelea.

Alisema Serikali



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato, akizungumza na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) wakati wa semina iliyoitanyika Septemba 24, 2022 jijini Dodoma.



Katibu Mkuu Wizara ya Nishati Mha. Felchesmi Mramba, akizungumza wakati wa Semina ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) iliyoitanyika Septemba 24, 2022 jijini Dodoma

imetenga sh. bilioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya kupoza umeme katika wilaya za Mkuranga, Tunduru, Mpanda, Mlele, Sikonge, Uvinza, Urambo, Ngara, Handeni, Bariadi, Ukerewe, Lushoto, Rombo, Kilindi na Kishatu ambapo ujenzi wa vituo hivyo utaanza mwezi Oktoba mwaka huu.

Byabato aliongeza kuwa, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) limefanya upembuzi yakinifu na kubaini maeneo yenye mahitaji

makubwa ambayo vituo hivyo vya kupoza umeme vitajengwa.

“Serikali imezingatia zaidi maeneo yenye changamoto kubwa ya upatikanaji wa umeme wa uhakika na hivyo Wizara tumeamua kuanza na hayo ili wananchi wapate umeme wa uhakika.” Alisema Byabato.

Alieleza kuwa, mwaka 2023/2024 TANESCO itaendelea kujenga vituo vya kupoza umeme kupitia mpango wake wa gridi imara katika maeneo

# SERIKALI YAAHIDI KUJENGA VITUO 15 VYA KUPOZA UMEME

yenye mahitaji ya kati ambayo hayakufikiwa katika awamu ya kwanza ya mradi.

“Lengo la Serikali ya Awamu ya Sita ni kuhakikisha kila mtanzania mwenye uhitaji wa kupata huduma ya umeme anafikiwa na huduma hiyo.” Alieleza

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhe. Felchesmi Mramba, alisema kuwa, Serikali inaendelea na mikakati mbalimbali ili kuhakikisha inasimamia

vyanzo vya kuzalisha umeme ukiwemo mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) pamoja na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Chalinze ambacho ujenzi wake unaendelea vizuri.

Naye, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dunstan Kitandula, alishauri Serikali kuongeza usimamizi wa ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere ili uweze kukamilika



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, Dunstan Kitandula, akizungumza wakati wa Semina ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) iliyofanyika Septemba 24, 2022 jijini Dodoma.

kwa wakati kutokana na umuhimu wa mradi huo kwa taifa.

Kitandula pia, aliisitiza Wizara ya Nishati kusimamia suala la utunzaji wa mazingira kwenye mradi huo na kusisitiza suala la upandaji miti kwenye maeneo ambayo yana uharibifu wa mazingira.

Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) wakiwa kwenye semina iliyoandaliwa na Wizara ya Nishati iliyofanyika Septemba 24, 2022 jijini Dodoma.



# WAZIRI MAKAMBA AZINDUA KIWANDA CHA TRANSFOMA

**W**aziri wa Nishati, January Makamba, Septemba 12, 2022 amezindua kiwanda cha kuzalisha transfoma ikiwa ni awamu ya pili ya kiwanda cha kuzalisha vifaa vya umeme cha Elsewedy Electrica Industrial Complex kilichopo

Kigamboni jijini Dar es Salaam.

Awamu ya kwanza ya kiwanda hicho inayohusisha utengenezaji wa nyaya za umeme ilizinduliwa Desemba 2021 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan.

Awamu ya pili ya

kiwanda hicho ambayo inahusisha uzalishaji wa transfoma itawezesha kiwanda kuwa na uwezo wa kuzalisha transfoma 2,500 kwa mwaka na kikitarajiwa kutengeneza ajira 1500.

Akizungumza wakati wa uzinduzi, Waziri Makamba alipongeza uwekezaji huo na kueleza Serikali

itaendelea kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji.

“Ni mafanikio makubwa kuona awamu ya pili ya kiwanda inakuja ikiwa ni miezi sita tu tangu kuanza kwa uzalishaji wa awamu ya kwanza,” alisema

“Hii inaonyesha kiasi gani mmedhamiria kufanya uwekezaji wenye tija. Upande wetu Serikali tutaendelea kuweka mazingira wezeshi



Waziri wa Nishati, January Makamba (wa Kwanza kulia) akizindua kiwanda cha kuzalisha transfoma ikiwa ni awamu ya pili ya kiwanda cha kuzalisha vifaa vya umeme cha Elsewedy Electric Industrial Complex kilichopo Kigamboni jijini Dar es Salaam. Wengine katika picha ni viongozi kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati na watendaji kutoka kampuni ya Elsewedy Electric.



# WAZIRI MAKAMBA AZINDUA KIWANDA CHA TRANSFOMA

kwa biashara,” alisema Makamba.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Elsewedy Electric East Africa, Ibrahim Qamar alisema uzalishaji huo wa transoma 2500 kwa mwaka unaweza

kuongezeka kulingana na uhitaji katika soko.

“Uzinduzi wa kiwanda cha transfoma unazidi kufungua milango ya ushirikiano kati ya Tanzania na Misri. Kiwanda hiki kitasaidia kuingiza

utalaam huu hapa Tanzania na kuwajengea uwezo watalaam wa hapa nchini,” alisema

“Ahadi yetu ni kwamba tutendelea kuzitafuta na kuziendeleza fursa ambazo zinaunga

mkono mpango mkakati wa kuendeleza viwanda nchini Tanzania,” alisema Qamar.

Kiwanda hicho kilichojengwa na kampuni ya wazawa ya Advent Construction Limited kinatarajia pia kupanua uzalishaji wake wa nyaya na transfoma sambamba na kuanzisha uzalishaji wa mita na PVC.



Waziri wa Nishati, January Makamba (Katikati) akiwa katika kiwanda cha kuzalisha transfoma cha Elsewedy Electric Industrial Complex kilichopo Kigamboni jijini Dar es Salaam. Wengine katika picha ni viongozi kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati na watendaji kutoka kampuni ya Elsewedy Electric.

# SERIKALI YAAHIDI KUANZA MRADI WA KUZALISHA UMEME WA RUMAKALI

**Na Timotheo Mathayo,**  
**Dodoma.**

**S**erikali imeahidi kuanza ujenzi wa mradi wa kuzalisha umeme wa Rumakali katika Wilaya ya Makete mkoani Njombe utakaozalisha Megawati 222.

Mradi huo utatekelezwa kupitia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ambapo maandalizi ya utekelezaji wa mradi huo yameanza kwa hatua za awali.

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato wakati akijibu swali la Mbunge wa Makete, Mhe.Festo

Sanga aliyetaka kujua ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Bwawa la umeme katika Mto Rumakali.

Swali hilo liliulizwa wakati wa mkutano wa Bunge uliomalizika jijini Dodoma, Ijumaa Septemba 23, 2022 ambapo Byabato alisema kuwa, Serikali imetenga sh.bilioni 8 kwa ajili ya maandalizi ya awali ya mradi huo katika mwaka wa fedha 2022/2023.

“TANESCO imehuisha upembuzi yakinifu pamoja na nyaraka za zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi mjenzi wa mradi huo”, alisema Byabato.

Alisema, uthamini wa mali za wananchi zitakazopitiwa na mradi huo utakamilika mwezi Oktoba, 2022 ili kuwezesha wananchi kulipwa fidia, hivyo utekelezaji wa mradi huo wa kuzalisha umeme unatarajia kuanza mwaka wa fedha 2023/2024.

Byabato alieleza kuwa, mradi wa kuzalisha umeme wa Rumakali utakapokamilika utawanufaisha wakazi wa Makete pamoja na maeneo mengine ya nchi kwa kuwa utaunganishwa kwenye gridi ya Taifa.

Byabato alisema, Serikali inaendelea kujenga vituo vya kuipoza umeme katika maeneo mbalimbali nchini ili kuweza kukabiliana na tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara.



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato.*



# WAZIRI MAKAMBA AKUTANA NA MABALOZI WA UINGEREZA, SINGAPORE



Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (Kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Balozi wa Uingereza nchini, Mhe. David Concar mara baada ya kumalizika kwa mazungumzo kati yao.

## Na Mwandishi Wetu

**W**aziri wa Nishati Mhe. January Makamba amekutana na kufanya mazungumzo na Mabalazi wa nchi za Uingereza na Singapore kwa nyakati tofauti

kuhusu ushirikiano baina ya nchi hizo na Tanzania kwenye maeneo mbalimbali ya sekta ya nishati.

Mazungumzo hayo yalifanyika Septemba 2, 2022 katika ofisi za Wizara ya Nishati jijini Dar es Salaam huku yakihudhuriwa na baadhi

ya viongozi wa Wizara .

Kwenye mazungumzo yake na Balozi wa Uingereza nchini, Mhe. David Concar, viongozi hao walijadili maeneo ya ushirikiano ambayo ni pamoja na kujengea uwezo wataalamu hususani katika kuhamasisha mpango

kabambe wa kuendeleza sekta ya umeme nchini (Power System Master Plan), kubadilishana uzoefu katika eneo la umeme na katika utekelezaji wa miradi ya umeme wa nishati jadidifu.

Waziri Makamba aliwakaribisha

# WAZIRI MAKAMBA AKUTANA NA MABALOZI WA UINGEREZA, SINGAPORE



Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (Kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Balozi wa Singapore nchini, Mhe. Douglas Foo mara baada ya kumalizika kwa mazungumzo kati yao.

wawekezaji wa nchini Uingereza kuwekeza kwenye miradi ya ujenzi wa njia za kusafirisha umeme (Independent Transmission Providers) pamoja na miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia nishati jadidifu.

Naye, Balozi Concar alisema Serikali ya Uingereza ipo tayari kutoa msaada kwa

Tanzania kwenye masuala ya kiufundi. Vivyo hivyo alisema Serikali hiyo ina nia ya kushirikiana na Tanzania kwenye masuala ya nishati bora ya umeme wa kupikia (electronic cooking).

Kwa upande mwingine, wakati wa mazungumzo kati ya Waziri Makamba na

Balozi wa Singapore, Douglas Foo, viongozi hao walijadili kuhusu uwezekano wa Tanzania kununua mafuta kutoka Singapore na ushirikiano katika miradi ya nishati jadidifu.

Balozi Foo alimtaarifu pia Waziri Makamba kuwa Serikali ya Singapore tayari imeshaanza kufanya

mazungumzo na wafanyabishara wa Tanzania kwa ajili ya kuwa na makubalino ya biashara, na kuongeza kuwa mwaka 2023, Singapore itatuma wataalamu wake kuja Tanzania ili kujadili maeneo mbalimbali ya uwekezaji na ushirikiano.



# Serikali kujenga vituo vya kupoza umeme katika wilaya zenye uhitaji

**Na Timotheo Mathayo,  
Dodoma.**

**S**erikali imeendelea na mkakati wa kutekeleza miradi ya kuimarisha huduma za upatikanaji wa umeme katika wilaya mbalimbali nchini Tanzania.

Kauli hiyo imetolewa na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato wakati akijibu swali la Mbunge wa Igunga, Nicholas Ngasa aliyetaka kujua ni lini Serikali itajenga kituo cha kupoza umeme cha Igunga.

Swali hilo liliulizwa wakati wa mkutano wa Bunge jijini Dodoma, Septemba 14, 2022.

Byabato alisema kuwa, Serikali kupitia TANESCO imebaini uhitaji wa vituo vya kupoza umeme katika Wilaya zenye uhitaji huo, pia imeweka mpango wa ujenzi wa vituo hivyo kulingana na uhitaji kuanzia mwaka huu wa fedha 2022/23.

Alisema ujenzi wa kituo kipya cha kupoza umeme cha Igunga kitawekwa katika mpango wa ujenzi wa Vituo vya kupoza umeme katika mwaka ujao wa



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato.*

fedha.

Aliongeza kuwa, ili kuimarisha huduma ya umeme katika Wilaya ya Igunga na Nzega, Serikali

inaendelea na mradi wa upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Lusu kilichopo wilayani Nzega kutoka MVA 15 132/33kV

hadi MVA 60 132/33kV na upanuzi huo unategemea kukamilika ndani ya mwaka huu wa fedha 2022/23.



## WAZIRI MAKAMBA AWAASA WABUNGE WANAWAKE KUHAMASISHA NISHATI BORA YA KUPIKIA

**Reuben Richard,  
Dodoma**

**W**aziri wa Nishati, Mhe. January Makamba amewaasa Wabunge Wanawake nchini kutoa elimu kwa wananchi kuhusu nishati bora ya kupikia ili kuweza kulisaidia Taifa kuepokana na Matumizi ya Nishati isiyosalama.

Alito wito huo Septemba 22, 2022 wakati wa semina maalum ya kuwajengea uwezo Wabunge Wanawake kuhusu nishati bora ya kupikia vijijini iliyofanyika jijini Dodoma.

Waziri Makamba aliwasihi Wabunge hasa wanawake wahakikishe wanaweka mikakati bora katika majimbo yao kama kutoa elimu juu ya Matumizi sahihi ya nishati ili kuweza kuokoa maisha ya wanawake na watu wote wanaotumia muda mwingi jikoni ambapo alitanabaisha kuwa, saa moja ya kutumia kuni ni sawa na kuvuta sigara mia tatu ambazo zinasababisha madhara makubwa ya kiafya.

"Kila Mbunge hasa nyie mama zetu tuhakikishe katika maeneo yetu tunawapa elimu ya kutosha



*Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba*

Wananchi ambao bado hawajanufaika na matumizi sahihi ya nishati mbadala kwa sababu moshi wa kuni na mkaa hauna tofauti na yule anayevuta sigara mia tatu kwa siku kwa sababu zote zinawaletea madhara makubwa

kwenye afya zao na kuharakisha vifo vyao na hata kupelekea tatizo la mimba zinazoishia katikati kama watoto kuzaliwa njiti au mimba kutoka kabla ya wakati."Alisisitiza

Alisema Serikali imeamua kulibeba

jambo hilo la uwepo wa nishati bora ya kupikia kwa ukubwa wake ili kubadilisha hali ya maisha ya wakina Mama kwa kuwaletea nishati mbadala na pia kuweza kuweka usawa kati ya walionacho na wasionacho.

Kwa Upande wake Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Edson Ngabo alisema kuwa nishati bora ya kupikia ikiwemo matumizi ya majiko ya gesi itakapotumika kikamilifu na kwa upana mkubwa sehemu mbalimbali nchini, itasaidia kuondokana na magonjwa yanayotokana na kutumia nishati isiyosalama.



*Sehemu ya Wabunge Wanawake wakifuatilia Hotuba ya Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (hayupo pichani) wakati wa Semina Maalum ya Kuwajengea Uwezo Wabunge Wanawake kuhusu Nishati Bora ya Kupikia vijijini iliyofanyika jijini Dodoma.*



# SERIKALI KUENZISHA OFISI MAALUM YA MRADI WA LNG

**W**aziri wa Nishati, Mhe. January Makamba, ametembelea ofisi za Kampuni ya Shell, nchini Uholanzi, na kukutana na kuzungumza na Viongozi Wakuu wa kampuni hiyo kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na utekelezaji wa mradi wa LNG nchini.

Katika mazungumzo hayo na Bwana Cederic Cremers, Makamu wa Rais anayeshughulikia miradi ya LNG na Bwana John Crocker, Makamu Rais wa Shell anayehusika na Mahusiano ya Serikali, Waziri Makamba alieleza azma ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ya kuhakikisha mazungumzo yanakamilika mwezi Disemba mwaka huu na hatua za utekelezaji zinaanza mara baada ya hapo.

Katika mikutano hiyo, Waziri Makamba pia alieleza mpango wa Serikali wa kuanzisha Ofisi Maalum ya Kusimamia Utekelezaji wa Mradi wa LNG (Tanzania LNG Office)

## MAZUNGUMZO KUKAMILIKA DISEMBA - WAZIRI MAKAMBA



*Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba (Wa Pili kushoto) akizungumza na Viongozi Wakuu wa kampuni ya Shell (kulia), Bw. Cederic Cremers, Makamu wa Rais anayeshughulikia miradi ya LNG na Bwana John Crocker, Makamu Rais wa Shell anayehusika na Mahusiano ya Serikali wakati Waziri Makamba alipotembelea Ofisi za Kampuni ya Shell, nchini Uholanzi, na kukutana na kuzungumza na Viongozi hao Wakuu kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na utekelezaji wa mradi wa LNG nchini.*

mnamo mwezi Novemba mwaka huu kwa lengo la kuratibu, kuharakisha na kurahisisha hatua za utekelezaji wa mradi.

Mradi huo wa kuchakata na kusindika gesi asilia iliyogundulika katika bahari kuu Kusini mwa Tanzania, utaleta nchini uwekezaji wenye thamani ya dola za Kimarekani bilioni 40, unatekelezwa na Makampuni ya Shell ya Uholanzi na Equinor ya Norway na washirika

wao.

Waziri Makamba alieleza kwamba mradi huo una manufaa mengi kwa Tanzania na utafungua fursa nyingi kwa wananchi wa Mikoja ya Kusini mwa Tanzania na kuiongezea mapato nchi na kuleta ajira na mapinduzi ya kiuchumi na kijamii nchini.

Kwa upande wa Kampuni ya Shell, Bw. Crocker, aliishukuru Serikali ya Awamu ya 6, inayoongwa na Rais

Samia Suluhu Hassan kwa kuwapa wawekezaji matumaini na kutoa kipaumbele katika mradi huo na kuwezesha kusainiwa kwa mkataba wa awali. Pia alieleza kuridhishwa kwao kwa hatua ya majadiliano iliyofikiwa katika maandalizi ya utekelezaji wa mradi huo. Bw. Crocker alisisitiza nia yao na ya washirika wao ya kutekeleza mradi.



## MITAA ISIYO NA UMEME HANDENI KUPATA HUDUMA HIYO IFIKAPO DESEMBA 2022

meelezwa kuwa, Mitaa 28 ambayo bado haina umeme katika Jimbo la Handeni mjini ipo katika mpango wa kupatiwa umeme kupitia mradi wa umeme vijijini Awamu ya Tatu mzunguko wa Pili unaotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Hayo yalisemwa Bungeni jijini Dodoma na Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato wakati akijibu swali la Mbunge wa Handeni Mjini, Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa ambaye aliuliza kuhusu mpango wa Serikali wa kupeleka umeme katika mitaa 28 ya Jimbo la Handeni Mjini ambayo bado haijapata umeme.

Naibu Waziri alisema kuwa, mitaa hiyo inapelekwa umeme na mkandarasi kampuni ya DERM ELECTRICS TANZANIA ambaye yupo katika eneo la kazi na anaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umeme katika maeneo mbalimbali ya Wilaya ya



*Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato.*

Handeni. Naibu Waziri aliongeza kuwa, Jimbo la Handeni Mjini lina jumla ya mitaa 60

ambapo kati ya mitaa hiyo, 32 ina umeme sawa na asilimia 53.3 na mitaa 28 haina umeme sawa asilimia 46.7.

Alisema kuwa kazi ya kupeleka umeme kwenye mitaa hiyo itakamilika Mwezi Desemba, 2022.



## Waziri Makamba ashiriki Warsha ya Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia nchini Norway

**W**aziri wa Nishati, Mhe. January Makamba, pamoja na Balozi wa Tanzania kwenye nchi za Nordic, Mhe. Grace Olotu na Balozi wa Norway nchini Tanzania, Mhe. Elisabeth Jacobsen wameshiriki katika Warsha ya Viongozi iliyofanyika kwenye Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia (Liquefied Natural Gas Plant - LNG) wa Equinor. Mradi huo upo Kaskazini mwa Norway kwenye mji wa Hammerfest.

Warsha hiyo iliyowashirikisha pia Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Bw. Kheri Mahimbali na uongozi wa juu wa kampuni ya Equinor, ilitoa nafasi kwa viongozi hao kujadili maandalizi ya mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia

Tanzania wenye thamani ya shilingi trilion 70 utakaofanyika mkoani Lindi.

Viongozi hao walitumia fursa hiyo kukutana na wafanyabiashara wa eneo hilo wanaonufaika kwa kutoa huduma kwenye eneo hilo la mradi wa Equinor, Hammerfest. Pia kukutana na Watanzania wanaofanya kazi katika mradi huo.

Mtambo uliojengwa kwenye mradi huo wa Equinor huchakata bilioni 4.6 za mita za ujazo za gesi asilia kwa mwaka ikiwa ni pamoja na bidhaa nyingine kama gesi ya kupikia (LPG).

Waziri Makamba aliwahakikishia Equinor na washirika wake kuwa Serikali ya Tanzania, chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, itaendelea kushirikiana nao ili kuhakikisha kuwa



Waziri wa Nishati, Mhe. January Makamba, pamoja na Balozi wa Tanzania kwenye nchi za Nordic, Mhe. Grace Olotu na Balozi wa Norway nchini Tanzania, Mhe. Elisabeth Jacobsen wakiwa kwenye mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia (Liquefied Natural Gas Plant - LNG) wa Equinor. Mradi huo upo Kaskazini mwa Norway kwenye mji wa Hammerfest.



Baadhi ya mitambo katika mradi wa kuchakata na kusindika gesi asilia (Liquefied Natural Gas Plant - LNG) wa Equinor. Mradi huo upo Kaskazini mwa Norway kwenye mji wa Hammerfest.

majadiliano yote ya msingi kuhusu Mradi wa Kuchakata na Kusindika

Gesi Asilia nchini yanakamilika ifikapo Desemba mwaka huu.



# JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI



**Fika Ofisi ya Mawasiliano,**  
Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au  
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018  
**Nukushi** +255-26-2320148

 [www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz)

 [Wizara ya Nishati](https://www.facebook.com/Wizara.ya.Nishati)

 [@Nishati2017](https://twitter.com/Nishati2017)

 [wizara\\_ya\\_nishati\\_tanzania](https://www.instagram.com/wizara_ya_nishati_tanzania)

 [Wizara ya Nishati](https://www.youtube.com/Wizara.ya.Nishati)